



## Nafasi za Kazi - Madereva (5)

Abacus Pharma (A) Ltd yenye makao makuu Dar es Salaam, Nyerere Kitalu 18C inajihusisha na uagizaji na usambazaji wa dawa za binadamu pamoja na vifaa tiba.

Wanahitajika madereva watano (5) wa kufanya kazi ndani ya mkoa wa Dar es Salaam wenye sifa zifuatazo:

### Sifa ya Muombaji:

- Leseni halali ya udereva na kufaulu katika madaraja A, A2, B, D & E.
- Awe Raia wa Tanzania mwenye akili timamu na umri usiopungua miaka 22.
- Elimu ya kidato cha nne (IV) na kuendelea.
- Awe amehitimu mafunzo ya udereva katika chuo kinachotambulika na Serikali.
- Uwezo wakwaida wa kuzungumza, kusoma na kuandika lugha ya Kiingereza.

### Majukumu ya Kazi:

- Kusambaza mizigo kwa wateja na vituo mbalimbali kama utakavyoelekezwa.
- Kuhakiki idadi ya mizigo inayopakwa na kushushwa katika chombo chako.
- Kukagua chombo kabla na baada ya kuanza safari ili kuhakikisha hali ya usalama wa chombo husika.
- Kutoa taarifa ya matengenezo yanayohitajika katika chombo unachokiendesha.
- Kuhakikisha chombo chako kipo katika hali ya usafi na ubora wakati wote tayari kwa matumizi.
- Kuhakikisha chombo chako kina vibali vyote vinavyohitajika na mamlaka mbalimbali.
- Kuweka katika kitabu cha kumbukumbu taarifa zote za safari unazozifanya kwa kutumia chombo chako.
- Kufanya majukumu mengine kadiri utakavyopangiwa na msimazi wako wa kazi.

### Jinsi Ya Kutuma Maombi:

Maombi yote yawasilishwe kupitia [apltz.recruitment@abacuspharma.com](mailto:apltz.recruitment@abacuspharma.com) kabla ya tarehe **23-03-2025**.

### Zingatia:

*"Abacus inatoa fursa sawa kwa wote na haiitaji mtu binafsi kulipa ada yoyote kama sehemu ya kupata upendeleo katika mchakato mzima wa kuajiri"*

**Inspired by Life**

Nyerere Road Plot 18C | [apltz.abacuspharma.com](mailto:apltz.abacuspharma.com) | P. O Box 13244 Dar es Salaam

Tel: +255 22 2865 212 / 213 | [www.abacuspharma.com](http://www.abacuspharma.com)